

**Annual Report 2024**  
*Ripoti ya Mwaka 2024*



**A REVIEW OF THE LAST YEAR**  
*MAPITIO YA MWAKA ULIOPITA*

## **Empowering a New Generation**

*Kuwezesha Kizazi Kipya*

[www.kijana-kwanza.org](http://www.kijana-kwanza.org)

# Contents

## *Maudhui*

**3**

**Welcome to Kijana Kwanza**

*Karibu Kijana Kwanza*

**4**

**UK Chair's Statement**

*Kauli ya Mwenyekiti wa Uingereza*

**5**

**TZ Chair's Statement**

*Kauli ya Mwenyekiti wa Tanzania*

**6**

**Kijana Kwanza in Numbers**

*Kijana Kwanza kwenye Takwimu*

**7**

**Child & Student Sponsorship**

*Ufadhili wa Watoto na Wanafunzi*

**8**

**Primary School + Case Study**

*Shule ya Msingi*

**9**

**Pre-Form 1 + Case Study**

*Mafunzo ya Awali ya Kidato cha Kwanza*

**10**

**Secondary School + Case Study**

*Shule ya Sekondari*

**11**

**Advanced Level + Case Study**

*Elimu ya Sekondari ya Juu*

**12**

**Vocational Training + Case Study**

*Mafunzo ya Ufundi na Uanagenzi*

**13**

**Technical Qualification + Case Study**

*Vigezo vya Kitaalamu*

**14**

**Extra-Curricular Learning**

*Mtaala wa Ziada na Elimu Isiyo Rasmi*

**15**

**Community Service & Interfaith Work**

*Huduma za Jamii & Ushirikiano wa Dini*

**16-17**

**Emergency Appeals**

*Rufaa za Dharura*

**18-19**

**New Children's Home**

*Makao Mapya ya Watoto*

**20**

**Shabaha Farm**

*Shamba la Shabaha*

**21**

**Other Updates**

*Taarifa Nyingine*

**22**

**International Volunteering + Case Study**

*Kujitolea Kimataifa*

**23-25**

**Say Hello to our Team**

*Shime kwa Timu Yetu*

**26-27**

**Tribute to the Fallen**

*Heshima kwa Walioanguka*

**28**

**Acknowledgements**

*Shukrani*

Front Cover: **Raymond Expery Marusu** (2004-2024) delivering food aid during Easter

*Raymond Expery Marusu (2004-2024) akigawa msaada wa chakula kipindi cha Pasaka*

# Welcome to Kijana Kwanza

*Karibu  
Kijana Kwanza*



Kijana Kwanza (Young People First) is a child and youth development charity that aims to empower a new generation of Tanzanians to become engaged, globally aware and economically independent citizens.

We achieve this by providing a safe environment for children and young people to grow, stay healthy and access formal and informal learning, vocational training and life skills.

Our ultimate goal is for children and young people to acquire the means and abilities to become leaders, activists and change-makers. In this way, they not only benefit themselves, but also their immediate and extended families, their local villages and communities, and society at large.

*Kijana Kwanza ni taasisi ya maendeleo ya watoto na vijana ambayo inakusudia kuwezesha kizazi kipya cha Watanzania kuwa raia walio na ufanisi, uelewa wa kimataifa, na uhuru wa kiuchumi.*

*Tunafanikisha kufanya hili kwa kutoa mazingira salama ya kukua kwa watoto na vijana, kuwa na afya nzuri, na kupata elimu rasmi na isiyo rasmi, mafunzo ya ufundi na ujuzi wa maisha.*

*Lengo letu kuu ni kuona watoto na vijana wanapata uwezo na njia za kuwa viongozi, wanaharakati na wahamasishaji wa mabadiliko. Kwa namna hii sio tu wananufaika wao wenyewe lakini pia familia zao za karibu na za mbali, vijiji na jamii zao kwa ujumla.*

# UK Chair's Statement



It has been an honour to take up the role of Chair of the UK Board of Trustees for Kijana Kwanza since January 2024. As I have got to know the organisation better during these past months, I have been truly impressed by the breadth and diversity of its work. Having worked in international development for over two decades, I find great warmth in Kijana Kwanza's perspective of humility, solidarity and its commitment to locally-led solutions to child poverty in Tanzania.

To help support the organisation build on the achievements of its first five years, I have been working to put in place a new Board of Trustees with the right mix of skills and experience to support the organisation across all aspects of its strategy and governance. This has seen the addition of four new Board members each of whom is already making an important contribution, working alongside longer standing Trustees. We are also focused on building a strong leadership structure that will best enable and nurture impact, while at the same time ensuring the long-term sustainability of the organisation.

As the year ends, we are turning towards developing a vision for the next five years, that will help to consolidate the services we provide and open new avenues for diversifying income and partnerships.

I look forward to supporting this journey in the years to follow and hope that you too, will be encouraged and inspired by the critical work undertaken by Kijana Kwanza.

**Jessica Banfield**

## Kauli ya Mwenyekiti wa Uingereza

*Ni heshima kubwa kuchukua jukumu la kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa Kijana Kwanza tangu Januari 2024. Hivyo, nimeweza kujua taasisi hii vyema kwa kipindi hiki cha miezi iliyopita, kwa kweli nimependezwa sana na wigo mpana wa kazi zake. Nikiwa na uzoefu wa zaidi ya miongo miwili katika maendeleo ya kimataifa, napata faraja kubwa katika mtazamo wa unyenyekevu, mshikamano, na kujitolea kwa taasisi ya Kijana Kwanza katika kutatua tatizo la umasikini kwa watoto nchini Tanzania kwa njia zinazoongozwa na jamii za ndani.*

*Ili kusaidia taasisi kujenga mafanikio yake ya miaka mitano ya mwanzo, nimeshiriki katika kuunda Bodi mpya ya Wadhamini yenye mchanganyiko mzuri wa ujuzi na uzoefu ili kusaidia taasisi katika nyanja zote za mikakati na utawala.*

*Hii imeleta wajumbe wanne wapya wa Bodi ambao kila mmoja tayari anatoa mchango muhimu, wakishirikiana na Wadhamini waliopo muda mrefu. Pia tumejizatiti katika kujenga muundo imara wa uongozi ambao utasaidia na kukuza athari, huku tukihakikisha ustawi wa kudumu wa taasisi.*

*Kadri mwaka unavyokaribia kumalizika, tunaelekea kuunda maono ya miaka mitano ijayo, ambayo yatasaidia kuimarisha huduma tunazotoa na kufungua njia mpya za kupata mapato na ushirikiano.*

*Natarajia kuunga mkono safari hii katika miaka ijayo na natumai hata nanyi mtahamasika na kuvutiwa na kazi madhubuti inayofanywa na Kijana Kwanza.*

**Jessica Banfield**

# TZ Chair's Statement



The past year has been one of incredible growth and development in our services, projects and activities. We now boast a local staff team of 38 members and a Senior Management Committee of 6 members who have worked alongside the Board of Trustees to improve and advance our mission in transforming lives.

Alongside new projects, such as the construction of our New Children's Home, and an expansion of Kariwa Shelter for Children & Young People and the opening of KK Workshop, we have dedicated significant efforts to developing a robust infrastructure to sustain our achievements for the long-term. This includes regular training for staff and volunteers, reviewing organisational policies and systems and exploring new methodologies for improving the quality of our work, and our ability to monitor and report on both the immediate and long-term outcomes of our interventions. As always, these efforts are work in progress, and sometimes quite novel in our cultural context, which require change management and adapting to new ways, but which we are committed to for the long-term.

As we present our report for the last year, I would like to remember our loved ones who passed away in a tragic accident in June 2024 (see page 26-27). Amongst the casualties was Raymond, a sponsored student of Kijana Kwanza, my nephews Mustapha and Ashrafu, and my dear wife Hadija, a teacher at Kijana Kwanza, who stood by me in fulfilling our aspirations to empower a new generation of children and young people in Tanzania. May they rest in peace.

**Mujibu Idrisa Abeid**

## Kauli ya Mwenyekiti wa Tanzania

Mwaka uliopita umejaa ukuaji na maendeleo makubwa katika huduma zetu, miradi na shughuli zetu. Sasa tunajivunia timu ya wafanyakazi wa hapa nchini yenye wanachama 38 na Kamati ya Usimamizi wa Juu yenye wanachama 6 ambao wamefanya kazi kwa karibu na Bodi ya Wadhamini kuboresha na kuendeleza dhamira yetu ya kubadilisha maisha

Pamoja na miradi mipya, kama vile ujenzi wa Nyumba ya Watoto ya Kisasa, upanuzi wa Kituo cha Kariwa cha Watoto na Vijana, na uzinduzi wa Karakana la KK, tumedhamiria kutoa jitihada kubwa katika kukuza miundombinu thabiti ili kudumisha mafanikio yetu kwa muda mrefu.

Hii inajumuisha mafunzo ya mara kwa mara kwa wafanyakazi na wanaojitolea, kupitia sera na mifumo ya taasisi na kuchunguza mbinu mpya za kuboresha ubora wa kazi zetu, pamoja na uwezo wetu wa kufuatilia na kuripoti matokeo ya haraka na ya muda mrefu ya shughuli zetu. Kama ilivyo kawaida, juhudi hizi ni kazi inayoendelea, na wakati mwingine ni mpya katika muktadha wetu wa kitamaduni, hivyo zinahitaji usimamizi wa mabadiliko na kujifunza njia mpya, lakini tumedhamiria kuendelea nazo kwa muda mrefu.

Tukiwa tunawasilisha ripoti yetu ya mwaka uliopita, ningependa kuwaenzi wapendwa wetu waliopoteza maisha kwa ajali ya kusikitisha mwezi Juni 2024 (angalia ukurasa 26-27). Miongoni mwa waliofariki alikuwa Raymond, mwanafunzi aliyefadhiliwa na Kijana Kwanza, wapwa zangu Mustapha na Ashrafu, na mke wangu mpendwa Hadija, aliyekuwa mwalimu wa Kijana Kwanza, ambaye alinisimamia kwa kutimiza malengo yetu ya kuwezesha kizazi kipya cha watoto na vijana nchini Tanzania. Wapumzike kwa amani.

**Mujibu Idrisa Abeid**

# Kijana Kwanza in Numbers

*Kijana Kwanza  
kwenye Takwimu*



**250**

Sponsored  
Students

*250 Wanafunzi  
Waliofadhiliwa*

**42**

New  
Graduates

*42 Wahitimu Wapya*

**12**

Operational Sites  
& Locations

*12 Sehemu za Uendeshaji  
na Mahali*

**385**

Children Received  
Medical Insurance

*385 Watoto Waliopokea  
Bima ya Afya*

**16,255**

Kilometres  
Travelled by our  
School Buses

*16,255 Kilomita  
Zilizotembewa na  
Mabasi Yetu ya Shule*

**178**

Learned Basic  
Computer Skills

*178 Walijifunza Ujuzi wa  
Msingi wa Kompyuta*

**134,310**

Eggs Laid on  
Shabaha Farm

*134,310 Mayai Yaliyozaishwa  
Shambani Shabaha*

**66,300**

Meals Served at  
Kijana Kwanza

*66,300 Milo iliyotolewa  
Kijana Kwanza*

**15**

Number of Interest  
Free Loans  
Provided

*15 Idadi ya Mikopo Isiyo  
na Riba Iliyotolewa*

**45,250**

Number of Bricks  
Used to Build New  
Children's Home

*45,250 Idadi ya Matofali  
Yaliyotumika Kujenga  
Nyumba Mpya ya Watoto*

**53**

Staff  
& Volunteers

*53 Wafanyakazi  
na Wanaojitolea*

**16,760**

Total Direct  
Beneficiaries

*120 Jumla ya Wanufaika  
wa Moja kwa Moja*

# Child & Student Sponsorship



Every year, we select a new cohort of children and young people to join our sponsorship programme through which they receive holistic and tailored support to overcome poverty and hardship, pursue education or vocational training and fulfil their potential and aspirations.

Our selection process is based entirely on need, rather than any specific academic ability or achievement, ensuring that we concentrate our resources on the most marginalised children and young people.

Once a child or young person is selected, they embark on a life journey with Kijana Kwanza and become part of our community. To ensure that young people are not left stranded midway through their education or training, we pledge to support sponsored students up to the point where they have the means to fend for themselves and become financially independent. As students “graduate” from Kijana Kwanza, we recruit new students to take their place.

The support we offer is tailored to the specific needs and circumstances of the child or young person. Some our sponsored children and young people live in single parent families or foster care in the community, whilst others may live on-site at one of our children’s homes or youth hostels. Where a young person would benefit from greater independence, he/she may be housed in private rented or college accommodation.

**Regardless of their living arrangements, we commit to provide each child and young person with:**

- a) a safe place to stay
- b) healthy and nutritious meals
- c) basic health insurance
- d) access to education or vocational training (including school meals, uniform and supplies)
- e) extra-curricular activities and life skills training
- f) pastoral care and support

**In the last year, a total of 250 children and young people between the ages of 5–25 years were sponsored by Kijana Kwanza.**

## *Ufadhili wa Watoto na Wanafunzi*

*Kila mwaka, tunachagua kundi jipya la watoto na vijana kujiunga na programu yetu ya ufadhili ambapo wanapata msaada wa kina na unaolengwa ili kudhibiti umaskini na ugumu wa maisha, kupata elimu au mafunzo ya ufundi na kufikia malengo na matarajio yao. Mchakato wetu wa kuchagua watoto unazingatia kabisa mahitaji, badala ya uwezo wa taaluma au mafanikio, kuhakikisha kuwa tunatumia rasilimali zetu kwa watoto na vijana wanaohitaji msaada zaidi.*

*Mara tu mtoto au kijana anapochaguliwa, anaanza safari ya maisha na Kijana Kwanza na kuwa sehemu ya jamii yetu. Ili kuhakikisha kuwa vijana hawaachwi njiani katikati ya elimu au mafunzo yao, tunajitolea kuwasaidia wanafunzi waliodhaminiwa hadi wanapokuwa na uwezo wa kujimudu na kuwa na uhuru wa kifedha. Wakati wanafunzi wanapohitimu Kijana Kwanza, tunachagua wanafunzi wapya kuchukua nafasi zao.*

*Msaada tunaoutoa, unatolewa kulingana na mahitaji na hali ya mtoto au kijana. Baadhi ya watoto na vijana wetu waliodhaminiwa wanaishi katika familia za mzazi mmoja au chini ya utunzwaji wa familia za kambo katika jamii, wakati mwingine wanaweza kuishi katika moja ya nyumba zetu za watoto au hosteli za vijana. Mahali ambapo kijana angefaidika na uhuru zaidi, anaweza kuishi katika makazi binafsi ya kupanga au makazi ya chuo.*

***Bila kujali mpangilio wa makazi yao, tunahakikisha tunampatia kila mtoto na kijana:***

- a) mahali salama pa kuishi
- b) chakula chenye afya na virutubisho
- c) bima ya afya
- d) Upatikanaji wa elimu au mafunzo ya ufundi (ikiwemo chakula cha shule, mavazi na vifaa)
- e) shughuli za ziada za elimu na mafunzo ya ujuzi wa maisha
- f) huduma za malezi na msaada

***Katika mwaka uliopita, jumla ya watoto 250 na vijana wenye umri wa miaka 5–25 walidhaminiwa na Kijana Kwanza.***

# Primary School + Case Study



This year, we admitted our first children and primary school age to Kijana Kwanza, following the closure of a local orphanage last year, which left them homeless. Whilst many were re-housed, the remaining students are now sponsored by the organisation. Whilst our primary school children currently live at Kariwa Shelter alongside our secondary school students, the new children's home under construction (refer to page 18-19) in Shabaha District will eventually provide more suitable premises for younger children.

Primary school children attend private schools, as opposed to government schools, where the medium of instruction is English, rather than Swahili. This ensures that children complete primary school with a good command of English, which is the language of instruction in secondary schools. Outside of school, the children enjoy a vibrant programme of informal learning, extra-curricular activities and play to broaden their personal, social and life skills.

This year, Kijana Kwanza sponsored 12 students of primary school age.

## BRAYAN'S STORY (10 years old)



***"My father became paralyzed after a motorcycle accident, and he cannot do anything but lie in bed, unable to help himself. After my father's accident my mother left me with my grandmother, and I don't know where she is. My grandmother could not look after me because she was very old, and so local government decided that I should stay at Kijana Kwanza. Now I am very happy."***

## Shule ya Msingi

Mwaka huu, Kijana Kwanza kwa mara ya kwanza tulidahili watoto wetu wa shule ya msingi, baada ya kufungwa kwa kituo cha watoto yatima mwaka jana, kuwafanya watoto hao wabaki bila makazi. Ingawa wengi walipata makazi mapya, wanafunzi waliobaki sasa wanadhaminiwa na taasisi yetu. Ingawa watoto wetu wa shule ya msingi wanaishi katika Makao ya Kariwa pamoja na wanafunzi wa shule ya sekondari, nyumba mpya ya watoto inayojengwa (tazama ukurasa 18-19) katika kata ya Shabaha itatoa makao bora zaidi kwa watoto wadogo.

Watoto wa shule ya msingi wanasoma shule binafsi, badala ya shule za serikali, ambapo lugha ya ufundishaji ni Kiingereza, badala ya Kiswahili. Hii inahakikisha kuwa watoto wanamaliza shule ya msingi wakiwa na ufanisi wa lugha ya Kiingereza, ambayo ni lugha ya ufundishaji katika shule za sekondari. Nje ya shule, watoto wanafurahia programu nzuri ya kujifunza isiyo rasmi, shughuli za ziada za kielimu na michezo ili kupanua ujuzi wao binafsi, kijamii na ujuzi wa maisha.

***Mwaka huu, Kijana Kwanza ilifadhili wanafunzi 12 wa umri wa shule ya msingi.***

## HADITHI YA BRAYAN (Umri wa Miaka 10)

*"Baba yangu aligongwa na pikipiki na kupooza, na hawezi kufanya chochote isipokuwa kulala kitandani, hawezi kujisaidia kwa chochote. Baada ya ajali ya baba yangu, mama yangu aliniacha na bibi yangu, na sijui yuko wapi. Bibi yangu hakuwa na uwezo wa kunilea kwa sababu alikuwa mzee sana, na hivyo serikali ya kijiji iliamua niishi Kijana Kwanza. Sasa hivi nina furaha sana."*



# Pre-Form 1 + Case Study



The transition from primary school to secondary school is particularly difficult in Tanzania because primary education is delivered in Swahili whilst English is the medium of instruction in secondary school. Culturally, it is also when some of the most disadvantaged children drop out of education, in particular those

that are orphaned, abandoned or suffering neglect.

Our Pre-Form 1 course, which runs for 12 weeks after the Primary School Leaving Examination (PSLE), is an intensive programme developed in-house with the aim of ensuring that children are motivated and ready to start secondary school. The curriculum focuses heavily on covering gaps in primary school knowledge, acquiring basic English language skills and learning themed vocabulary relating to core curriculum subjects.

At the start of the course, children sit a pre-course examination to assess their understanding and provide a benchmark for their learning. At the end of the course, they sit a similar examination.

**This year, the average score in pre-course tests was 30%, rising to 66% at the end of the programme, demonstrating an improvement in 36 percentage points.**

**A total of 50 students were sponsored by Kijana Kwanza to attend the Pre-Form 1 course, with 28 students selected for full sponsorship through secondary school.**

## AZIZA'S STORY (13 years old)



*"When I was 4 years old, my father died and since my mother had cancer, I was taken to live with my grandmother. Since my grandmother had no job because of her old age, someone from the village took me in and paid for me to finish primary school. This year, I finished primary school and the man returned me to my grandmother. She is now very old and asked for help from social services, who requested Kijana Kwanza to help me. I am now doing the Pre-Form 1 course and hope that I will be selected to continue to secondary school."*

## Mafunzo ya Awali ya Kidato cha Kwanza

Mabadiliko kutoka shule ya msingi kwenda shule ya sekondari ni jambo gumu sana Tanzania kwa sababu elimu ya msingi hutolewa kwa Kiswahili, wakati Kiingereza ni lugha ya ufundishaji katika shule za sekondari. Kitamaduni, pia ni wakati ambapo baadhi ya watoto masikini wanatoka kwenye mfumo wa elimu, hasa wale ambao ni yatima, waliotelekezwa au wanaotelekezwa.

Kozi yetu ya mafunzo ya awali ya Kidato cha Kwanza, inayodumu kwa wiki 12 baada ya Mitihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE), ni programu ya kina iliyoandaliwa ndani ya taasisi kwa lengo la kuhakikisha kuwa watoto wanachochewa na kuwa tayari kuanza shule ya sekondari. Mtaala huu unalenga sana kuziba mianya ya maarifa ya shule ya msingi, kupata ujuzi wa msingi wa Kiingereza na kujifunza misamati inaohusiana na masomo ya mtaala mkuu.

Mwanzoni mwa mafunzo, watoto wanafanya mtihani wa awali wa tathmini ya ufahamu wao na kutoa kigezo cha kujifunza. Mwishoni mwa mafunzo, wanafanya mtihani mwingine wa aina hiyo.

**Mwaka huu, alama ya wastani katika mitihani ya awali ilikuwa 30%, ikiongezeka hadi 66% mwishoni mwa programu, ikiashiria ongezeko la alama kwa asilimia 36.**

**Jumla ya wanafunzi 50 walidhaminiwa na Kijana Kwanza kuhudhuria mafunzo ya awali ya Kidato cha Kwanza, na wanafunzi 28 walichaguliwa kwa udamini kamili wa shule ya sekondari.**

## HADITHI YA AZIZA (umri wa miaka 13)

"Nilipokuwa na umri wa miaka 4, baba yangu alifariki na kwa vile mama yangu alikuwa na kansa, nilichukuliwa kwenda kuishi na bibi yangu. Kwa vile bibi yangu hakuwa na kazi kwa sababu ya umri wake mkubwa, msamaria mwema kutoka kijijini alinichukua na alilipa ada ili nimalize shule ya msingi. Mwaka huu, nilimaliza shule ya msingi na mtu huyo alinirudisha kwa bibi yangu. Kwa sasa bibi yangu ni mzee sana na aliomba msaada ustawi wa kijamii, ambao waliomba Kijana Kwanza kunisaidia. Sasa nasoma mafunzo ya awali ya Kidato cha Kwanza na nina matumaini kwamba nitachaguliwa kuendelea na shule ya sekondari."

# Secondary School + Case Study



Adolescence is one of the most challenging times for a vulnerable child or young person, when there is greater risk of school drop-out, delinquency and marginalisation. The choices that a young person makes between the ages of 12-18 years can have a huge impact, positive or negative on their future lives. As a result, secondary school students represent the largest cohort of our sponsored students.

Not all our children are academically gifted, and whilst some perform extraordinarily well, others may struggle, in particular due to their social circumstances and past experiences. As a result, we invest significant resources invested in additional tuition, particularly during the holidays, and organise wide ranging extra-curricular activities that enhance their wider skills, regardless of whether they decide to continue to Advanced Level or consider alternative training options after secondary school.

**This year, Kijana Kwanza sponsored 139 students of secondary school age. A total of 126 students passed their end of year examinations (representing 90.65%) with 28 students achieving Division 1 (equivalent to Grade A\*).**

## FREDRICK'S STORY (16 years old)



*"My father died just before I was born and so my mother, still pregnant, took over my father's business, making charcoal in an outdoor furnace and selling to local villagers. It was hard work and she was struggling. My mother proposed to other men so that a man could provide for us, but each time they cheated her and left her pregnant. We are now 3 children, and my mother cannot provide for us to go to school. Because of Kijana Kwanza, I am now in secondary school and I hope that one day I can provide for my family."*

## Shule ya Sekondari

Kipindi cha kubalehe ni mojawapo ya nyakati ngumu kwa mtoto au kijana aliye hatarini, ambapo kuna hatari kubwa ya kuacha shule, uhalifu na kutengwa. Maamuzi ambayo kijana hufanya kati ya umri wa miaka 12-18 yanaweza kuwa na athari kubwa, nzuri au mbaya, kwa maisha yao ya baadaye. Hivyo basi, wanafunzi wa shule ya sekondari wanawakilisha kundi kubwa la wanafunzi wetu waliofadhiliwa.

Sio watoto wetu wote wana uwezo wa kitaaluma, na ingawa wengine wanafanya vizuri sana, wengine wanapambana, hasa kutokana na hali zao za kijamii na mambo waliyopitia awali. Matokeo yake, tunatumia rasilimali nyingi kwa ajili ya masomo ya ziada, hasa wakati wa likizo, na tunaratibu shughuli mbalimbali za ziada za elimu zinazoboresha ujuzi wao wa kijamii, bila kujali kama wataamua kuendelea na ngazi ya juu ya elimu au kuzingatia chaguzi nyingine za mafunzo baada ya shule ya sekondari.

Mwaka huu, Kijana Kwanza ilidhamini wanafunzi 139 wa shule ya sekondari. Jumla ya wanafunzi 126 walifaulu mitihani yao wa mwisho wa mwaka (ikiwa ni sawa na 90.65%) na wanafunzi 28 walipata Division 1 (sawa na Daraja A\*).

## HADITHI YA FREDRICK (umri wa miaka 16)

*"Baba yangu alifariki kabla ya mimi kuzaliwa, hivyo mama yangu, akiwa mjamzito, alichukua biashara ya baba yangu, akichoma mkaa kwenye tanuru na kuuza kwa wanakijiji. Ilikuwa kazi ngumu na alikuwa anateseka. Mama yangu alijaribu kuolewa na wanaume wengine ili waweze kutunza familia yetu, lakini mara zote walimdanganya na kumwacha akiwa mjamzito. Sasa tupo watoto 3, na mama yangu hana uwezo wa kutupeleka shule. Kwa sababu ya Kijana Kwanza, sasa nipo shule ya sekondari na nina matumaini kwamba siku moja nitaweza kutunza familia yangu."*

# Advanced Level + Case Study



Sponsored students who perform well in secondary school examinations are selected by government to attend Advanced Level education in a combination of 3 subjects, depending on their individual interests and performance.

Government schools that deliver Advanced Level education are boarding schools, and students may be selected to attend school in any region of the country. During term-time, Advanced Level students live in their respective schools, returning to our youth hostel during holidays where they receive additional private tuition to support their learning.

Most of our Advanced Level students will progress to university at which point their sponsorship ends as they can normally access government loans for higher education.

This year, Kijana Kwanza sponsored 12 students to pursue Advanced Level education. A total of 7 students achieved Division 1 (equivalent to Grade A\*) or Division 2 (equivalent to Grade A/B) in their mid-year or end of year examinations, representing 58.33% of the total number of sponsored students.

## NEEMA'S STORY (19 years old)



*"My father died from HIV/AIDS and our extended family took all our land and property because my parents were not married, and my mother was forced to leave the village. I was left abandoned and moved to Moshi, where my sister's friend allowed me to stay for a short while. After finishing primary school, I had nowhere to go until Kijana Kwanza sponsored me and placed me with a foster family. This enabled me to complete secondary school and now I am in my final year of Advanced Level, studying Economics, Commerce and Accountancy. I hope to go to university next year."*

## Elimu ya Sekondari ya Juu

Wanafunzi waliofadhiliwa wanaofanya vizuri katika mitihani ya shule ya sekondari wanachaguliwa na serikali kujiunga na elimu ya sekondari ya juu kwa kuchagua michepuo ya masomo 3, kulingana na maslahi yao binafsi na ufaulu wao.

Shule za serikali zinazotoa elimu ya sekondari ya juu ni shule za bwani, na wanafunzi wanaweza kuchaguliwa kusoma katika mkoa wowote nchini. Kipindi cha masomo, wanafunzi wa elimu ya sekondari ya juu wanaishi katika shule zao, na wanarudi katika hosteli yetu ya vijana wakati wa likizo ambapo wanapewa masomo binafsi ya ziada ili kusaidia kujifunza kwao.

Wanafunzi wetu wengi wa kidato cha tano na sita watasonga mbele kwenda chuo kikuu, ambapo ufadhili wao utamalizika kwani wanapata mikopo ya serikali kwa ajili ya elimu ya juu.

**Mwaka huu, Kijana Kwanza ilifadhili wanafunzi 12 kupata elimu ya sekondari ya juu. Jumla ya wanafunzi 7 walipata Divisheni 1 (sawa na Daraja A\*) au Divisheni 2 (sawa na Daraja A/B) katika mitihani yao ya katikati ya mwaka au ya mwisho wa mwaka, ikiwa ni 58.33% ya jumla ya wanafunzi waliofadhiliwa.**

## HADITHI YA NEEMA (umri wa miaka 19)

"Baba yangu alifariki kwa ugonjwa wa UKIMWI na wanafamilia wetu wengine walichukua ardhi na mali zetu kwa sababu wazazi wangu hawakuwa wamefunga ndoa, na mama yangu alilazimishwa kuondoka kijijini. Nilitekelezwa na nilihamia Moshi, ambapo rafiki wa dada yangu aliniruhusu nikae kwake kwa muda. Baada ya kumaliza shule ya msingi, sikuwa na mahali pa kwenda hadi Kijana Kwanza iliponifadhili na kuniweka katika familia ya kambo. Hii iliniwezesha kumaliza shule ya sekondari na sasa niko mwaka wangu wa mwisho wa masomo ya sekondari ya juu, nikisomea Uchumi, Biashara na Uhasibu. Nina matumaini ya kwenda chuo kikuu mwakani."

# Vocational Training + Case Study



For school dropouts and those young people less inclined to formal education in a school or college setting, our vocational training and apprenticeship programme offers an alternative route to gaining skills that enable young people to learn a trade and becoming financially independent.

At the start of the year, we acquired a rent-free warehouse in Moshi Town, which has now been converted into a workshop where tradesmen and technicians deliver courses in mechanics, tailoring, electrical installation, welding and carpentry. We are also piloting an outcomes-based curriculum to demonstrate learning in an informal environment.

Due to the size of the facility and its ability to accommodate large numbers of students, we have also opened up the workshop to young people sponsored by other local organisations to acquire practical training.

**This year, Kijana Kwanza sponsored 20 students to pursue vocational training. We also supported an additional 9 external trainees with practical skills at our new workshop.**

## NASMA'S STORY (21 years old)



*"Last year, my father passed away after he accidentally took some medication which caused his blood pressure to fall to a fatal level. My mother was left to care for all of us – my older sister who has no job, and my 2 younger siblings who are still in school. After I finished secondary school, I did not have many options until I came to learn about Kijana Kwanza. Here I am studying to be a mechanic, which is unusual for a girl in our society, but I know I can earn a good income afterwards and provide for my family."*

## Mafunzo ya Ufundi na Uanagenzi

Kwa watoto walioacha shule na vijana ambao hawaonyeshi hamu ya elimu rasmi katika mazingira ya shule au chuo, programu yetu ya mafunzo ya ufundi na uanagenzi inatoa njia mbadala ya kupata ujuzi ambao utawasaidia vijana kujifunza biashara na kuweza kujitegemea kifedha.

Mwanzoni mwa mwaka, tulipata ghala lisilo na kodi ndani ya Mji wa Moshi, ambalo sasa linatumika kama karakana ambapo mafundi na wahandisi wanatoa mafunzo ya ufundi stadi wa magari, ushonaji, ufundi umeme, kuchomelea na useremala. Pia tunajaribu mtaala unaozingatia matokeo ili kuonesha namna ya kujifunza katika mazingira yasiyo rasmi.

Kwa sababu ya ukubwa wa kituo hiki na uwezo wake wa kuweza kubeba idadi kubwa ya wanafunzi, pia tumeweza kufungua sehemu ya mafunzo kwa vitendo kwa ajili ya vijana wanaofadhiliwa na taasisi nyingine za hapa ili kupata mafunzo kwa vitendo.

**Mwaka huu, Kijana Kwanza ilifadhili wanafunzi 20 kusoma mafunzo ya ufundi. Pia, tulisaidia wanafunzi 9 kutoka nje kwa ajili mafunzo ya vitendo katika karakana yetu mpya.**

## HADITHI YA NASMA (umri wa miaka 21)

*"Mwaka jana, baba yangu alifariki baada ya kumeza dawa kwa bahati mbaya ambayo ilisababisha shinikizo lake la damu kushuka hadi kiwango cha hatari. Mama yangu alibaki kutulea sisi sote – mimi, dada yangu mkubwa ambaye hana kazi, na wadogo zangu wawili ambao bado wanasoma. Baada ya kumaliza shule ya sekondari, sikuwa na chaguo jingine mpaka pale nilipojua kuhusu Kijana Kwanza. Hapa nasomea ufundi magari, jambo ambalo si la kawaida kwa msichana katika jamii yetu, lakini najua nitaweza kupata kipato kizuri baada ya kumaliza na kuisaidia familia yangu."*

# Technical Qualification + Case Study

Many of our school graduates consider pursuing a technical qualification as a quicker and more focused route to employment.

College-based technical qualifications have lower entry requirements than university and can also be an alternative to Advanced Level education, whilst still offering the opportunity to progress to university.

Currently, we are sponsoring 19 students studying a range of disciplines including Clinical Medicine, Pharmaceutical Sciences, ICT, Nursing, Business Administration, Electrical Engineering, Veterinary Science, Nursing, Midwifery, and Social Work.

**This year, we also celebrated our first graduates who completed healthcare-related qualification.**



## Vigezo vya Kitaalamu

Wahitimu wetu wengi wa shule wanachukulia kusoma ujuzi wa kiufundi kama njia ya haraka na yenye umakini zaidi ya kupata ajira. Sifa za kiufundi zinazohitajika kwa ajili ya kujiunga na vyuo zina mahitaji madogo ya kujiunga kuliko vyuo vikuu na pia zinaweza kuwa mbadala wa elimu ya Kidato cha tano na sita huku bado zikitoa fursa ya kuendelea na masomo ya chuo kikuu.

Kwa sasa, tunafadhili wanafunzi 19 wanaosoma fani mbalimbali ikiwemo Kliniki tiba, Sayansi ya Dawa, Tecknolojia ya Habari na Mawasilino, Uuguzi, Usimamizi wa Biashara, Uhandisi wa Umeme, Sayansi ya Mifugo, Ukunga, na Ustawi wa jamii

**Mwaka huu, pia tulisherehekea wahitimu wetu wa kwanza waliomaliza fani zinazohusiana na huduma za afya.**

## SAMWEL'S STORY (24 years old)



*"After my father died, our stepmother stole our inheritance, including our livestock. In Masai culture, we depend on our livestock and so it was difficult for me to continue my education. I spent a while helping other Masai in the village look after their livestock, but my dream was always to become a veterinarian. Kijana Kwanza gave me that opportunity, and I expect to graduate at the end of the year. I have also been offered a 1 year placement in Denmark next year, which is an amazing opportunity for any Tanzanian."*

## HADITHI YA SAMWEL (umri wa miaka 24)

*"Baada ya baba yangu kufariki, mama yetu wa kambo alituibia urithi wetu, ikiwemo mifugo yetu. Katika tamaduni za Wamasai, tunategemea mifugo yetu na hivyo ilikuwa vigumu kwangu kuendelea na masomo yangu. Nilikaa kwa muda nikisaidia Wamasai wengine kijijini kutunza mifugo yao, lakini ndoto yangu ilikua kuwa daktari wa mifugo. Kijana Kwanza ilinipa fursa hiyo, na ninatarajia kuhitimu mwishoni mwa mwaka huu. Pia nimepewa nafasi ya kufanya kazi kwa mwaka mmoja nchini Denmark mwaka ujao, ambayo ni fursa kubwa mno kwa Mtanzania yeyote."*

# Extra-Curricular Learning



Alongside formal education, we emphasise the holistic development of the children in our care. Children are encouraged to adopt positive habits such as personal hygiene, good behaviour and regular house chores, which are rewarded through a points-based pocket money scheme. During evenings and weekends, we deliver a regular programme of additional activities including sports, workshops, interactive games, lively debates and community service that aim to both entertain and broaden the knowledge and horizons of children and young people.

## Some examples of activities during the last year:

- Slam Poetry Competition: A platform for students to express themselves through the art of performance poetry.
- Cultural Culinary Exchange: An evening of international cookery skills led by international volunteers.
- Nutrition and Fitness: Workshops to promote a healthy lifestyle through nutrition, fitness, and relaxation techniques.
- Employability: A comprehensive programme including CV writing, interview skills, and practical job readiness training.
- First Aid: Training in first aid techniques preparing young people for emergency situations.
- Stress and Time Management: Practical seminar to help students manage stress and improve their time management skills.
- Arts and Crafts: Creative workshops included traditional weaving, mixed media self-portraits, lino printing, clay modelling and calligraphy.
- Literacy and Numeracy: Fun and practical outdoor games to make literacy and numeracy learning enjoyable.
- Sexual Health Education: Informative sessions covering topics related to reproductive health.
- Mental Health Awareness: Workshops aimed at raising awareness about mental health.
- Film Screening: A discussion on women's issues in Tanzania as portrayed in the film "Binti", addressing topics such as gender-based violence, societal pressures and family dynamics.

## Mtaala wa Ziada na Elimu Isiyo Rasmi

*Pamoja na elimu rasmi, pia tunazingatia maendeleo ya jumla ya watoto katika huduma zetu. Watoto wanahimizwa kuiga tabia njema kama vile usafi binafsi, tabia nzuri na kazi za nyumbani za kawaida, ambazo zinatunukiwa kupitia mfuko wa pesa ya matumizi inayotolewa kwa kuzingatia alama. Wakati wa jioni na mwisho wa wiki, tunatekeleza ratiba ya kawaida ya shughuli za ziada ikiwa ni pamoja na michezo, semina, michezo ya kuburudisha, midahalo hai na huduma za jamii ambazo zina lengo la kuburudisha na kupanua maarifa na upeo wa watoto na vijana.*

### **Baadhi ya mifano ya shughuli zilizofanyika mwaka huu:**

- Shindano la Kughani Shairi: Ni jukwaa kwa ajili ya wanafunzi kujieleza kupitia sanaa ya utumbuizaji wa mashairi.
- Upishi wa Vyakula vya Kitamaduni: Ni jioni ya stadi za kupika za kimataifa ziliongozwa na wageni wetu wa kimataifa.
- Lishe na Mazoezi: Ni semina za kukuza maisha yenye afya kupitia lishe, mazoezi na mbinu za kujipumzisha.
- Uwezo wa Kuajiriwa: Ni programu kamili ikihusisha uandishi wa CV, mbinu za usahili na mafunzo ya vitendo ya maandalizi ya kazi.
- Huduma ya Kwanza: Mafunzo ya mbinu za huduma ya kwanza huwaandaa vijana kwa matukio ya dharura.
- Usimamizi wa Mkazo na Muda: Warsha za vitendo za kusaidia wanafunzi kudhibiti mkazo na kuboresha ufanisi wao wa kuzingatia muda.
- Sanaa na Ufundi: Warsha za ubunifu ikiwa ni pamoja na ufumaji wa kitamaduni, picha binafsi zilizochanganywa, uchapaji wa lino, ufinyanzi na sanaa ya uandishi.
- Uwezo wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu: Michezo ya vitendo ya furaha inayosaidia kufurahia kujifunza hesabu, kusoma na kuandika.
- Elimu ya Afya ya Uzazi: Vipindi vya taarifa vinavyohusu mada zinazohusiana na afya ya uzazi.
- Utambuzi wa Afya ya Akili: Warsha zinazolenga kuongeza ufahamu kuhusu afya ya akili.
- Kuonyesha Filamu: Mijadala kuhusu masuala ya wanawake Tanzania kama inavyoonyeshwa kwenye filamu ya "Binti", inahusu masuala kama vile ukatili wa kijinsia, shirikizo la kijamii na mienendo ya familia.

# Community Service & Interfaith Work

## Huduma za Jamii & Ushirikiano wa Dini



Kijana Kwanza is a non-denominational organisation, and an equal number of Christian and Muslim children and young people benefit from sponsorship and the different services we provide. We provide prayer facilities to accommodate the needs of all our children, who are encouraged to learn more about their faith and develop their spirituality.

Alongside our deepest respect for the needs of different faith communities, we also prioritise interfaith social action as a means of creating a unified generation of Tanzanian youth who are ready to serve, without distinction.

Centred around religious festivals, Christians and Muslims at Kijana Kwanza celebrate, commemorate and serve together. Over Easter and Ramadan, our children packed and hand delivered over 620 food parcels to poor families and on Eid al-Adha and Christmas Day, we invited over 100 young people to participate in our festivities, which included sports and entertainment.

*Kijana Kwanza ni taasisi isiyo ya kidini, na watoto wa Kikristo na Waislamu wanafaidika sawa na udhamini na huduma mbalimbali tunazotoa. Tunatoa vifaa vya kuswalia ili kukidhi mahitaji ya watoto wetu wote, ambao wanahimizwa kujifunza zaidi kuhusu imani zao na kujikuzi kiroho.*

*Pamoja na heshima yetu kubwa kwa mahitaji ya jamii mbalimbali za kidini, pia tunasisitiza hatua za kijamii za kidini kama njia ya kuunda kizazi chenye ushirikiano cha vijana wa Kitanzania ambao wako tayari kuhudumia bila kujali tofauti za kidini.*

*Kuhusu sherehe za kidini, Wakristo na Waislamu wa Kijana Kwanza wanasherehekea, kukumbuka na kuhudumu pamoja. Wakati wa Pasaka na Ramadhani, watoto wetu walipakia na kugawa vifurushi 620 vya chakula kwa familia masikini, na kipindi cha sikukuu ya Eid al-Adha na Sikukuu ya Krismasi, tulialika vijana zaidi ya 100 kushiriki sherehe zetu, ambazo zilijumuisha michezo na burudani.*

# Emergency Appeals: Market Fire

At the start of the year, a ferocious fire engulfed Mbuyuni Market, in the centre of Moshi Town. Hundreds of small vendors and traders lost their entire stock of fruit and vegetables, leaving them without any means to earn a living.

The majority of these traders were single mothers, living below the poverty line. On a good day, they would make a profit of just TZS. 3,000 (£1/US\$1.3), hardly enough to feed their children. Already struggling families, lost everything.

Following a meeting with the District Commissioner of Moshi Town, Kijana Kwanza launched an emergency appeal to assist small traders with dependent children.

**With the support of donors and sponsors from across the world, we distributed 120 cash grants to enable traders to restart their businesses, alongside emergency food parcels and basic supplies for the immediate relief of their families.**

## Rufaa za Dharura: Moto Sokoni

*Mwanzoni mwa mwaka, moto mkali uliteketeza Soko la Mbuyuni, katikati ya Mji wa Moshi. Maelfu ya wafanyabiashara wadogo walipoteza bidhaa zao zote za matunda na mboga, wakiachwa bila njia ya kujipatia riziki.*

*Wengi wa wafanyabiashara hawa walikuwa wakina mama masikini. Ambao katika siku nzuri za mauzo, wangeweza kupata faida ya TZS 3,000 (Pauni 1 / Dola ya Marekani 1.3), ambayo haitoshi hata kuwalisha watoto wao. Tayari familia ambazo zinateseka, zimepoteza kila kitu.*

*Baada ya mkutano na Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kijana Kwanza ilianzisha ombi la dharura ili kuwasaidia wafanyabiashara wadogo wenye watoto ambao wanawategemea.*

*Kwa msaada wa wahisani na wafadhili kutoka duniani kote, tuligawa ruzuku 120 za pesa kusaidia wafanyabiashara kuanzisha upya biashara zao, pamoja na vifurushi vya chakula cha dharura na vifaa vya msingi kwa msaada wa haraka kwa ajili ya familia zao.*





# Emergency Appeals: Flood Relief

In April 2024, heavy rains in Moshi Town and surrounding villages and districts caused rivers and streams to break their banks, resulting in devastating floods in low lying areas. Bridges collapsed, home were washed away, and crops destroyed. In one incident, a mud slide collapsed the roof of a house, killing 3 children.

Amongst those affected by the floods were sponsored children of Kijana Kwanza living in the community.

**In response, our staff and volunteers were at the forefront of the relief work. This included the distribution of 25 emergency food parcels, 100 mattresses and 3 cash grants for families in need of finding alternative accommodation.**



## Rufaa za Dharura: Msaada kipindi cha Mafuriko

Mwezi Aprili 2024, mvua kubwa zilizonyesha mjini Moshi, vijiji na wilaya zinazozunguka zilisababisha mito na mifereji kuvunja kingo zake, na kusababisha mafuriko makubwa katika maeneo ya bondeni. Madaraja yalidondoka, nyumba zilichukuliwa na mafuriko, na mazao kuharibiwa. Katika tukio moja, maporomoko ya udongo yalibomoa paa la nyumba, na kuua watoto watatu.

Kati ya walioathiriwa na mafuriko hayo walikuwa watoto wanaofadhiliwa na Kijana Kwanza wanaoishi kwenye jamii.

**Katika hilo, wafanyakazi wetu na wahudumu walikuwa mstari wa mbele katika kazi ya msaada. Hii ilijumuisha ugawaji wa vifurushi vya chakula vya dharura 25, magodoro 100 na ruzuku za pesa 3 kwa familia zinazohitaji msaada wa kupata makazi mbadala.**

# New Children's Home

## Makao Mapya ya Watoto

### Tatizo

Inakadiriwa kuwa na yatima 1,300,000 na watoto wa mitaani 437,000 nchini Tanzania. Matokeo yake, vituo vya Watoto yatima na makao ya watoto vilivyojisajili kisheria vimejaa kupita kiasi na vinashindwa kukidhi idadi ya watoto. Hii imesababisha kuongezeka kwa makao yasiyosajiliwa ambapo watoto wanyonge wanaishi katika hali duni na wakati mwingine wanakuwa wahanga wa unyonyaji na unyanyasaji.

Kijana Kwanza sasa inanzisha upya mfumo wa ustawi kwa watoto yatima na waliotelekezwa wenye umri wa miaka 5-12. Baada ya kununua kiwanja cha ekari 1 katika kata ya Shabaha mwishoni mwa mwaka 2023, tumeanza kujenga makao ya watoto, makubwa zaidi katika Mkoa wa Kilimanjaro.



## The Problem

There are an estimated 1,300,000 orphans and 437,000 street children in Tanzania. As a result, legally registered orphanages and children's homes are severely overcrowded and struggling to absorb the numbers. This has led to the proliferation of unregistered establishments where vulnerable children live in squalor and are sometimes subject to exploitation and abuse.

Kijana Kwanza is now reinventing the welfare model for orphaned and abandoned children aged 5-12 years. Following the purchase of a 1-acre plot in Shabaha District at the end of 2023, we have started construction of a new children's complex, the largest in Kilimanjaro Region.

# New Children's Home

## Makao Mapya ya Watoto

### Why is this project different?


We believe that children aged 5-12 years should grow up in a loving family. Where a child has been abandoned due to poverty, we will prioritise family reunification, by supporting the family unit to stay together or place the child in a foster family. The new children's home will operate as an emergency shelter – and only in the most challenging circumstances will children be kept in long-term care on-site.

Once placed in community care, families will continue to receive financial and in-kind support, scheduled and surprise home visits from social workers and children will attend weekly activities on-site at the children's home.

### Kwa nini mradi huu ni wa kipekee?

Tunaamini kwamba watoto wenye umri wa miaka 5-12 wanapaswa kukua katika familia yenye upendo. Pale ambapo mtoto ametelekezwa kwa sababu ya umaskini, tutapendelea kurudisha familia pamoja kwa kuwasaidia familia hiyo kubaki pamoja au kumuweka mtoto katika familia ya kambo. Nyumba mpya ya watoto itakuwa makao ya dharura – na ni katika mazingira magumu ya watoto ndipo watoto watakuwepo kwenye huduma za muda mrefu ndani ya makao.

Baada ya kuwekwa kwenye huduma za jamii, familia zitapata msaada wa kifedha na vitu, ziara za kushtukiza za nyumbani zitakazofanywa na mhudumu wa ustawi wa jamii na watoto watahudhuria shughuli za kila wiki katika nyumba ya watoto.



The total cost of the project is £750,000/\$995,000 of which 65% of funds have already been pledged or raised. We look forward to welcoming the first children to our new Children's Home in the second half of 2025.

Jumla ya gharama za mradi ni £750,000/\$995,000 ambapo 65% ya fedha tayari zimeahidiwa au kukusanywa. Tunatarajia kuwakaribisha watoto wa kwanza kwenye Nyumba yetu Mpya ya Watoto katika nusu ya pili ya mwaka 2025.

# Shabaha Farm



Two years ago, Kijana Kwanza acquired a 7-acre plot in Shabaha District, with the aim of growing our own produce and becoming food sustainable in 5 years.

In the past year, we have expanded our team and have 3 full-time farmers working and living on-site. Through their efforts, we have diversified our crops and have harvested a wide range of fruits, vegetables and grains, with an annual estimated value of TSH. 3,840,000 (£1263.64 /\$1585.06).

We have also now completed construction of a cow shed that is home to 7 dairy cows (and 3 calves) and a poultry barn that houses 658 chickens. Every week, our livestock produce an average of 182 litres of milk and 3780 eggs, which are used across all our sites, with the surplus sold at market.

We expect to build on this success over the next few years to increase our annual yield and meet our internal food needs and generate a regular income for the charity.

Separately, we have purchased a 1-acre plot in Hai District, which has now been fenced and will be used to breed goats, so that we have a regular supply of meat. We are currently appealing for funds to dig a bore hole and invest in the initial livestock of 100 goats.

## Shamba la Shabaha

Miaka miwili iliyopita, Kijana Kwanza ilinunua kiwanja cha ekari 7 katika kata ya Shabaha, kwa lengo la kuzalisha mazao yetu wenyewe na kuwa na Chakula cha kujitoshereza katika kipindi cha miaka 5.

Katika mwaka uliopita, tumeongeza timu yetu na sasa tuna wakulima 3 wa kudumu wanaofanya kazi na kuishi kituoni. Kupitia juhudi zao, tumeongeza aina za mazao na tumekusanya matunda, mboga na nafaka nyingi, ambazo thamani ya kila mwaka inakadiriwa kuwa TSH. 3,840,000 (£1263.64 /\$1585.06).

Pia sasa tumekamilisha ujenzi wa banda la ng'ombe ambalo linahifadhi ng'ombe wa maziwa 7 (na 3 ndama) na banda la kuku lenye kuku 658. Kila wiki, mifugo yetu huzalisha wastani wa lita 182 za maziwa na mayai 3780, ambayo hutumika kwenye maeneo yetu yote, na ziada inauzwa sokoni.

Tunatarajia kujenga zaidi kwenye mafanikio haya katika miaka michache ijayo ili kuongeza mavuno yetu ya kila mwaka na kukidhi mahitaji yetu ya chakula ya ndani na kupata mapato ya taasisi.

Pia, tumenunua kiwanja cha ekari 1 katika Wilaya ya Hai, ambacho kimezungushiwa uzio na kitatumika kuzalisha mbuzi, ili kuwa na usambazaji mdogo wa nyama. Hivi sasa tunachangisha fedha ili kuchimba kisima na kuwekeza kwenye mifugo ya awali ya mbuzi 100.

# Other Updates

# Taarifa Nyingine



## Back to School Appeal

With hundreds of children failing to report to school at the start of the year because they cannot afford essential school supplies, we provided 100 children with back to school packs to ensure that they could start or continue their education.

## Medical Insurance Appeal

Our annual Gift of Good Health Campaign ensured that 385 children and young people received basic medical insurance to promote good health and protect them from curable conditions including malaria, typhoid and stomach ulcers.

## Study Café

Our Study Café continues to be a popular venue for children and young people to study and access education resources. On average, 84 children and young people attended our Study Café on a weekly basis.

## Computer Classes

In the last year, 178 students have attend computer classes at Kijana Kwanza, the only site in Moshi Town where children and young people can access digital learning free of charge.

## Expansion of Kariwa Shelter

With the support of an international philanthropist, we received funding to expand Kariwa Shelter by constructing an additional 3 storey building to expand capacity for 28 students, as well as new staff accommodation, communal spaces for events and activities and a computer room.

### **Msaada wa Kurudi Shuleni**

*Kwa mamia ya watoto wanaoshindwa kuripoti shuleni mwanzoni mwa mwaka kwa sababu hawawezi kumudu vifaa muhimu vya shule, tuligawa paketi za kurudi shule kwa watoto 100 ili kuhakikisha wanaweza kuanza au kuendelea na masomo yao.*

### **Msaada wa Bima ya Afya**

*Kampeni yetu ya zawadi ya Afya Njema ya kila mwaka ilihakikisha kwamba Watoto 385 na vijana walipata bima ya afya ya msingi ili kuhakikisha wanakuwa na afya nzuri na kuwalinda dhidi ya magonjwa yanayoweza kutibika ikiwa ni pamoja na malaria, typhoid na vidonda vya tumbo.*

### **Mkahawa wa Kusomea**

*Sehemu yetu ya kujisomea inaendelea kuwa mahali maarufu kwa watoto na vijana kusoma na kupata rasilimali za elimu. Kwa wastani, watoto na vijana 84 walihudhuria sehemu yetu ya kujisomea kila wiki.*

### **Darasa la Kompyuta**

*Katika mwaka uliopita, wanafunzi 178 wamehudhuria mafunzo ya kompyuta yanayotolewa Kijana Kwanza, mahala pekee ndani ya Mji wa Moshi ambapo watoto na vijana wanaweza kupata masomo ya kidijitali bure kabisa.*

### **Upanuzi wa Makao ya Kariwa**

*Kwa msaada wa kifedha wa kimataifa, tulipokea fedha za kupanua makao ya Kariwa kwa kujenga jengo la ghorofa 3 kuongeza uwezo wa kubeba wanafunzi 28, pamoja na makazi mapya ya wafanyakazi, maeneo ya shughuli na matukio ya kijamii na chumba cha kompyuta.*

# International Volunteering + Case Study




This year, we welcomed 13 international guests to volunteer at Kijana Kwanza from different parts of the world including Europe and the Middle East!

**Volunteers were involved in a range of activities including:**

- Teaching formal curriculum subjects such as English, Maths & Science
- Delivering sports coaching
- Planting, harvesting and tending to livestock on Shabaha Farm
- Facilitating lectures, seminars and workshops
- Overseeing extra-curricular learning including arts, crafts, music and games
- Providing professional mentoring for staff and teachers

## **RAYAAN'S STORY** (16 years old)



*"I will never forget my time in Tanzania volunteering at Kijana Kwanza. I was able to make many friendships with the orphans at the shelter and was shown utmost hospitality. During the placement, I was truly inspired by the hardworking and determined nature of the children and their passion, appreciation and commitment to their education. I was fortunate enough to aid in the distribution food for the impoverished in the local area, as well as teaching Maths to secondary school students. I even had the chance to join the young people on a field trip, but if you want to play football at Kijana Kwanza, beware. They're good, and pretty competitive on the pitch."*

## *Kujitolea Kimataifa*

*Mwaka huu, tulikaribisha wageni 13 kutoka sehemu mbalimbali za dunia kujitolea ndani ya Kijana Kwanza, ikiwa ni pamoja na Ulaya na Mashariki ya Kati!*

***Wageni hao walijihusisha na shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na:***

- Kufundisha masomo rasmi kama vile Kiingereza, Hisabati na Sayansi
- Kutoa mafunzo ya michezo
- Kupanda, kuvuna na kutunza mifugo kwenye Shamba la Shabaha
- Kutoa mihadhara, semina na warsha
- Kusimamia masomo ya ziada ikiwa ni pamoja na sanaa, ufundi, muziki na michezo
- Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wafanyakazi na walimu

## **HADITHI YA RAYAAN** (umri wa miaka 16)

*"Sitosahau wakati wangu nchini Tanzania nikijitolea ndani ya Kijana Kwanza. Nilifanikiwa kufanya urafiki mkubwa na watoto yatima makaoni na nilipokelewa kwa ukarimu mkubwa. Kwa kipindi hiki, niliguswa sana na bidii, dhamira, shauku na utayari wa watoto hawa kwa ajili ya elimu yao. Nilifanikiwa kusaidia kugawa chakula kwa familia maskini katika eneo la jirani, pamoja na kufundisha Hisabati kwa wanafunzi wa shule ya sekondari. Nilikuwa na bahati ya kushiriki na vijana katika uwanja wa michezo, lakini ikiwa unataka kucheza mpira wa miguu Kijana Kwanza, basi jua kwamba wao ni wazuri na ni washindani sana uwanjani."*

# Say Hello to our Team

We are very proud of our local team of staff and volunteers who play an incredible role in managing our projects, running activities and overseeing the welfare of our children and young people.



**Abdul**  
Farmer



**Abushiri**  
Driver



**Alex**  
Security



**Amina**  
Cook (Kariwa Shelter)



**Aziza**  
Student Support  
Worker



**Batuli**  
Vocational  
Training Manager



**Brenda**  
Finance Intern




**Bui**  
Security (Workshop)



**Elia**  
Security (Moshi Town)



**Erick**  
Business Development  
Manager



**Fatuma**  
Maths Teacher



**Goodluck**  
Caretaker  
(Kariwa Shelter)

## Shime kwa Timu Yetu

*Tunajivunia sana timu yetu ya wafanyakazi wa ndani na wanaojitolea ambao wanafanya jukumu kubwa katika kusimamia miradi yetu, kuendesha shughuli na kusimamia ustawi wa watoto wetu na vijana.*

**Abdul**  
Mkulima

**Abushiri**  
Dereva

**Alex**  
Mlinzi

**Amina**  
Mpishi (Makao ya Kariwa)

**Aziza**  
Msimamizi wa Watoto

**Batuli**  
Meneja wa Mafunzo ya Ufundi

**Brenda**  
Mkurufunzi wa Masuala ya Fedha

**Bui**  
Mlinzi (Karakana)

**Elia**  
Mlinzi (Moshi Mjini)

**Erick**  
Meneja wa Maendeleo ya Biashara

**Fatuma**  
Mwalimu wa Hesabu

**Goodluck**  
Msimamizi wa vifaa na Mazingira  
(Makao ya Kariwa)

# Say Hello to our Team



**Gloria**  
Children's Services  
Manager



**Hadija**  
Student Support  
Worker



**Hassan**  
Driver



**Idrisa**  
Farmer



**Ivetha**  
Cleaner (Moshi Town)



**Juma**  
Education &  
Training Manager



**Kisra**  
Computer Teacher



**Kusunia**  
Social Work Intern



**Masoud**  
Student Support Worker



**Mohammed**  
Social Work Intern



**Mwajuma**  
Finance Manager



**Omary**  
Caretaker (Moshi Town)



**Ombeni**  
Farmer



**Rajabu**  
Driver



**Rajabu**  
Senior Student  
Support Worker

## Shime kwa Timu Yetu

### **Gloria**

Meneja wa Huduma za Watoto

### **Hadija**

Msimamizi wa Wanafunzi

### **Hassan**

Dereva

### **Idrisa**

Mkulima

### **Ivetha**

Mfanyaji Usafi (Moshi Mjini)

### **John**

Meneja wa shamba na Msimamizi  
wa miradi ya vijijini

### **Juma**

Meneja wa Elimu na Mafunzo

### **Kisra**

Mwalimu wa Kompyuta

### **Kusunia**

Mkurufunzi wa Masuala ya kijamii

### **Masoud**

Msimamizi wa Wanafunzi

### **Mohammed**

Mkurufunzi wa Masuala ya kijamii

### **Mwajuma**

Meneja wa Fedha

### **Omary**

Mlinzi wa Mchana (Moshi Mjini)

### **Ombeni**

Mkulima

### **Rajabu**

Dereva

### **Rajabu**

Msimamizi Mkuu wa Watoto



# Say Hello to our Team



**Regan**  
Social Welfare Officer



**Rehema**  
Finance Intern



**Retus**  
Outreach & Marketing  
Manager



**Sadath**  
Acting COO



**Saidi**  
Assistant Academic  
Officer



**Subira**  
Children's  
Support Worker




**Ulfah**  
Student Support Worker




**Ummy**  
Cook (Moshi Town)



**Yasini**  
Finance Officer



**Yusuph**  
Facilities Manager



**Zulfa**  
Cook (Kariwa Shelter)

...and many more volunteers and helpers.

## Shime kwa Timu Yetu

**Regan**  
*Afisa Ustawi wa jamii*

**Rehema**  
*Mkurufunzi wa Masuala ya Fedha*

**Retus**  
*Meneja Masoko na Uendeshaji*

**Sadath**  
*Mkurugenzi Mtendaji*

**Saidi**  
*Mtaaluma Msaidizi*

**Subira**  
*Msimamizi wa Watoto*

**Ulfah**  
*Msimamizi wa Watoto*

**Ummy**  
*Mpishi (Moshi Mjini)*

**Yasini**  
*Muhasibu*

**Yusuph**  
*Meneja wa vifaa*

**Zulfa**  
*Mpishi (Makao ya Kariwa)*

*...na wengine wengi wanaojitolea  
na wasaidizi.*

# Tribute to the Fallen

On the evening of **Saturday 29 June 2024**, we received tragic news that members of staff, their family members and a sponsored student of Kijana Kwanza, were involved in an accident.

Returning from Bukoba to Moshi, the vehicle was passing Tabora to drop off Raymond to boarding school, where he was due to start his A-Levels in Economics, Geography and Mathematics the following week. The group were accompanying Raymond to bid farewell, when the car crashed.

Pictures from the scene show a mangled car, blood-stained doors and bodies flung on the side road. Raymond and Mujibu, our Chair's nephews, Ashrafu and Mustapha, died instantly. Two members of staff were taken to hospital in a critical condition.

Word spread fast and heart-wrenching cries and wails echoed the walls of Kijana Kwanza. Across social media, our young people shared their memories and pictures of Raymond, as well as Ashrafu and Mustapha, who were regular visitors at Kijana Kwanza.

The following day, as Ashrafu and Mustapha were laid to rest in Bukoba, we gathered for an interfaith memorial service in the grounds of Kariwa Shelter, to remember the fallen. Consolata sang hymns Shabani read the Qur'an. Juma hugged me, crying uncontrollably.



At night, the children and young people of Kijana Kwanza started the 6-hour journey, passing Babati, where they met Raymond's coffin and joined the funeral procession to his final resting place in Kondo, his ancestral village. But as morning approached, we received news of the fourth

# Heshima kwa Walioanguka

Jioni ya **Jumamosi 29 Juni 2024**, tulipokea habari za majonzi kuwa wafanyakazi wetu, watu wa familia zao na mwanafunzi aliyefadhiliwa na Kijana Kwanza walipa ajali.

Kurejea kutoka Bukoba kuja Moshi, gari lilikuwa linapita Tabora kumpeleka Raymond shuleni ya bwani, ambapo alitarajiwa kuanza masomo yake ya kidato cha tano na sita katika masomo ya Uchumi, Jiografia na Hesabu wiki inayofuata. Kundi hilo lilikuwa linamsindikiza Raymond na kumuaga, ndipo gari lilipopata ajali.

Picha kutoka kwenye Tukio zinaonesha gari lililoharibiwa vibaya, damu mlangoni na miili iliyotupwa kando ya barabara. Raymond, wapwa wa Mwenyekiti wetu, Ashrafu na Mustapha, walifariki papo hapo. Wafanyakazi wawili walikimbizwa hospitalini wakiwa katika hali mbaya.

Habari zilisambaa haraka na vilio vya majonzi vilijaa kila kona ya Kijana Kwanza. Kwenye mitandao ya kijamii, vijana wetu walisambaza kumbukumbu na picha za Raymond, pamoja na Ashrafu na Mustapha, ambao walikuwa wageni wa mara kwa mara Kijana Kwanza.

Kesho yake, Ashrafu na Mustapha walizikwa Bukoba, wafuasi wa dini tofauti tulikusanyika kwa ajili ya ibada ya ukumbusho katika uwanja wa makao ya Kariwa, kuwakumbuka marehemu. Consolata aliimba tenzi za rohani. Shabani alisoma Qur'an. Juma alinikumbatia, akilia kwa uchungu.

Usiku wa siku hiyo, watoto na vijana wa Kijana Kwanza walianza safari ya takribani masaa 6, wakipitia Babati, ambapo walikutana na jenze la Raymond na kuungana na msafara wa mazishi hadi kwenye mapumziko yake ya mwisho huko Kondo, kijiji kwao. Lakini wakati kunakucha, tulipokea habari ya kifo cha nne; Hadija, mwalimu wa Kijana Kwanza, alikuwa amefariki kutokana na majeraha makubwa aliyopata. Baada ya kumzika Raymond, basi la shule lilianza safari ya saa 18 kwenda Bukoba kuhudhuria mazishi ya Hadija.

Bila shaka, ilikuwa wiki ngumu zaidi katika historia yetu.

Kwa taasisi inayofanya kazi kama familia, inamaanisha kwamba maafa kama haya, yanapotokea yanatugusa sisi sote. Na matukio ya wiki hiyo yalithibitisha kuwa sisi ni familia, sio muundo wa ushirika ambao ulipoteza safu chache za ngazi. Licha ya ukuaji wetu kwa miaka kadhaa, maadili hayo yameendelea kubaki.

Tangia hapo, Abushir, mfanyakazi mwingine, alifanyiwa upasuaji na matibabu kadhaa, na anaendelea kupona kwa haraka.

# Tribute to the Fallen

fatality; Hadija, a teacher at Kijana Kwanza, had succumbed to her injuries. After laying Raymond to rest, the school bus started the 18-hour journey to Bukoba to attend her funeral.

It was, without doubt, the most difficult week in our history.

When an organisation operates as a family, it means that a tragedy like this, breaks us all. And the events of that week proved that we are indeed a family, not a corporate structure that lost a few rungs of the ladder. Despite our growth over the years, that ethos remains.

Since then, Abushir, another member of staff, has undergone multiple operations and treatments, and is making a strong recovery.

Despite our grief, we are not defeated. Our goal and ambitions are no less important today than they were before this tragedy. We are committed to rescuing more children who have been orphaned, abandoned or abused and transforming the fortunes of young people who want to better their lives and become financially independent in the future.

That will never stop. And the memories of Raymond, Ashrafu, Mustapha and Teacher Hadija will inspire us every step of the way.

**May they rest in peace. I will miss them dearly.**

**Mohammed S Mamdani**  
Country Director



## Heshima kwa Walioanguka

*Licha ya majonzi yetu, hatujashindwa. Lengo na matamania yetu hayawezi kupungua kamwe kama ilivyokuwa kabla ya msiba huu. Tumejizatiti katika kuokoa watoto zaidi ambao ni yatima, wametengwa au kuteswa na kubadilisha maisha ya vijana wanaotaka kuboresha maisha yao na kuweza kujitegemea kifedha siku zijazo.*

*Hilo halitakoma kamwe. Na kumbukumbu za Raymond, Ashrafu, Mustapha na Mwalimu Hadija zitatuhamasisha kwa kila hatua.*

**Wapumzike kwa amani. Nitawakumbuka sana.**

**Mohammed S Mamdani**  
Mkurugenzi wa Nchi



# Acknowledgements

We would like to express our sincere thanks to the following companies and organisations that have supported our work over the last year:

## Shukrani

*Tunapenda kutanguliza shukrani zetu za dhata kwa kampuni zifuatazo na taasisi ambazo zimetusaidia kwenye kazi zetu kwa mwaka uliopita:*

Moshi Municipal Council

Lady Fatemah Charitable Trust

A F Dahya Family Foundation

Exim Bank

Lamabuild Ltd

TaxAssist Accountants

Silver Birch Care Ltd

Crescent Real Estate Ltd

Expert Tuition Ltd

Orison Charitable Trust

Quest Travel Limited

HMJK Architects

Hasnain Foundation

Freedom Traders (Dar es salaam)

Bilal Muslim Mission (Moshi)

Ally & Co

Beta Charitable Trust

BW Foundation

Chemist Click Ltd

Sabat Accountants

Sasate Ltd

Zanzibar International  
Development Organisation

Vyspa Ltd

Free Pentecostal Church Tanzania  
(Moshi)

Youth Empowerment &  
Psychotherapy Aid (Moshi)

### Kijana Kwanza

**Address:**

PO Box 261, Ghalla Road,  
Moshi, Tanzania

**Telephone/WhatsApp:**  
+255 754 544 203

**Email:**  
admin@kijana-kwanza.org

...and 1,427 individual donors

...na wafadhili mmoja mmoja 1,427